MAENDELEO YA KIMAUDHUI KATIKA TAMTHILIA TANO ZA EBRAHIM N. HUSSEIN.

Na: MUTEGI MUKOBWA, J.N.

"Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya 'Master of Arts' katika Chuo Kikuu cha Nairobi".

1985

Mukobwa, J N Mutegi
Maendeleo ya
kimaudhui katika

88/174435

UNGAMO

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine chochote"

Mutegi Mukobwa, J.N.
(Mtahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu".

Dkt. Jay Kitsao

Dkt. Muhamed Bakari

YALIYOMO

		UKURASA
Yaliyomo.....		i
Shukrani.....		iii
Muhtasari.....		v
SURA YA KWANZA		
1:1	Utangulizi.....	1
1:2	Somo la Utafiti.....	1
1.3.	Kusudi la Tasnifu.....	5
1:4	Upeo wa Somo Hili.....	7
1:5	Msingi wa Nadharia.....	14
1:6	Yaliyoandikwa kuhusu somo hili...	21
1:7	Sababu za kulichagua Somo Hili....	29
1:8	Njia za Utafiti.....	32
1:9	Tanbihi	33
SURA YA PILI		
2:1	Uhakiki wa Fasihi.....	35
2:2	Uhakiki unahusu Nini?.....	35
2:3	Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.....	36
2:4	Uhakiki wa Tamthilia,.....	44
2:5	Tanbihi.....	47
SURA YA TATU		
3:1	Kinjeketile.....	49
3:2	Utangulizi.....	49
3:3	Msingi wa Kihistoria.....	55

UKURASA

3:4	Athari za Kiuchumi kwa Watanzania.....	59
3:5	Mwanzo wa Vita vya Maji Maji.....	63
3:6	Maudhui Makuu katika Kinjeketile.....	67
3:7	Kiishilio	84
3:8	Tanbihi.....	87

SURA YA NNE

4:1	Wakati Ukuta na Alikiona.....	89
4:2	Utangulizi.....	89
4:3	Msingi wa Kihistoria.....	91
4:4	Maudhui Makuu katika Wakati Ukuta.....	95
4:5	Maudhui Makuu katika Alikiona.....	103
4:6	Kiishilio.....	107
4:7	Tanbihi.....	110

SURA YA TANO

5:1	Mashetani na Arusi.....	111
5:2	Utangulizi.....	111
5:3	Msingi wa Kisiasa na Kiuchumi.....	113
5:4	Maudhui Makuu katika Mashetani.....	126
5:5	Maudhui Makuu katika Arusi.....	143
5:6	Kiishilio.....	153
5:7	Tanbihi.....	156
5:8	HITIMISHO.....	158
	MAREJELEO.....	161

MUHTASARI

Uhakiki wa kazi yoyote ya fasihi unadhamiria kuchangia fasihi hiyo. Yampasa **kila** mhakiki aelewe kazi anayoihakiki kabla ya kuishughulikia. Manufaa ya mchango wake katika uwanja huu utategemea lengo lake na **kile** adhamiriacho kukifafanua. Hana budi basi kuwa na'**vifaa**' vya kumwezesha atekeleze wadhifa wake. Anahitaji kuwa na vigezo fulani anavyovitumia iwapo angetaka umuhimu wa kazi yake **udhihirike.**

Tasnifu hii ni juu ya uhakiki wa tamthilia tano za Kiswahili zilizoandikwa na Ebrahim N. Hussein baina ya mwaka wa 1967 na mwaka wa 1981. Tumeugawanya uhakiki huu katika sura tano. Hata hivyo uhakiki wa tamthilia zenyewe umechukua sura tatu. Hivi ni kusema kwamba tumeziweka tamthilia tano tunazozijadili katika sehemu tatu kulingana na umuhimu wake wa kimaudhui. Tamthilia nne kati ya hizi zimeshughulikiwa katika sehemu mbili kwa sababu mbili muhimu. Kwanza kuna kipindi cha kihistoria kinachojadiliwa na pili, ni kwa sababu ya kulingana kwa maudhui.Kulingana huku ni katika uzito ama udhaifu wa kimaundui. Kipimo cha kuamua udhaifu ama uzito huu ni msingi wa nadharia ya ki-Marx kuhusu fasihi. Hii ni nadharia inayosisitiza umuhimu wa maudhui katika kazi ya fasihi. Kila mojawapo ya sura tatu za mwisho ina Kiishilio kinachotoa muhtasari wa sura hiyo na pia uamuzi wa jumla kuhusu tamthilia iliyojadiliwa ama zilizojadiliwa. Mwisho kuna Hitimisho ambamo mnatolewa muhtasari wa viishilio vyote na maoni juu ya kazi zilizojadiliwa.

Sura ya kwanza ni utangulizi unaofafanua madhumuni ya tasnifu na hali kadhalika sababu za kulichagua somo hili. Pia msingi wa nadharia umeelezwa kwa jumla. Sura ya pili inafafanua zaidi unachohusu uhakiki pamoja na kueleza uhakiki wa tamthilia na fasihi kwa jumla. Sura hii ndiyo inayotongoa nadharia ya uhakiki wa kifasihi ambayo imezingatiwa katika tasnifu hii.

Sura ya tatu inahakiki tamthilia ya Kinjeketile. Pia kuna kidokezo juu ya msingi wa Kihistoria kudhihirisha kwamba tamthilia hii ina maudhui ya kihistoria. Hii ni tamthilia ambayo inazingatia tukio muhimu katika historia ya Watanzania. Tukio hili ni vita vya Maji Maji dhidi ya ukoloni wa Kijerumani. Sura hii inajaribu kuonyesha kwamba hivi vilikuwa vita kupinga mfumo wa kibepari uliojitokeza kwa sura ya ukoloni.

Tamthilia za Wakati Ukuta na Alikiona zimehakikiwa katika sura ya nne. Tamthilia hizi mbili zinalingana kimaudhui kwa kuwa zinazungumzia matokeo ya athari za mfumo wa kiuchumi na kibepari chini ya ukoloni mambo-leo.

Sura ya mwisho ni uhakiki wa Mashetani na Arusi ambazo zinajadili maswala mazito ya kiuchumi, kisiasa, kiitikadi na kiutamaduni katika muktadha mpana zaidi. Hizi ni tamthilia zenye mawazo mazito yaliyoshughulikiwa kijazanda. Katika Hitimisho, licha ya kutoa muhtasari na uamuzi wa jumla kuhusu tamthilia zilizojadiliwa, kuna pendekezo juu ya uhakiki wa fasihi ya kiswahili kwa jumla kama mojawapo ya njia za kukuza lugha ya Kiswahili.